

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SWALI LA 1

SURA YA TAHARIRI

Insha hii iwe na sehemu zifuatazo

- (i) Kichwa
 - a. Jina la gazeti
 - b. Tarehe
 - c. Mada

(ii) Utangulizi

(iii) Mwili

(iv) Hitimisho

Sehemu hii iwe na:

- (a) Jina la kampuni inayochapisha gazeti
- (b) Jina la cheo cha mhariri

Swali la kwanza

Baadhi ya hoja

1. Wananchi wana uoga watakuwa watumwa wa mataifa na mashirika haya.
2. Mikopo huja na masharti yaani baadhi ya masharti yanaumiza / hayafaidi taifa letu. Kwa mfano; kuwaajiri wafanyakazi kutoka nje k.v china.
3. Huenda ikaillemea taifa letu hivyo basi mauzo yetu / biashara zitakuwa hazina faida.
4. Kutawaliwa na mataifa au masharika ya kifedha. Kwa mfano, masharti tutakayowekewa k.v kupunguza idadi ya wafanyakazi wa serikali ilhali idadi ya watu inaendelea kukua.
5. Biashara zetu na mataifa haya zitaathirika. Yatakuwa yakinunua kwa bei watakayotaka kwa hivyo sisi ndio tutawahitaji zaidi.
6. Kuingilia uhuru wetu hata wa biashara. Wananchi wa mataifa hayo na mashirika hayo ya kifedha wataanza kufanya biashara zinazotakikana kufanywa na wenyeji m.f Wachina.
7. Asilimia kubwa ya mapato yetu itagharamia ulipaji wa mikopo na kutuacha tukiwa wategemezi wa shirika na mataifa hayo.

Swali la pili

Kuunga

- 2(a) Huleta ajira kwa vijana katika mashirika hayo ya kamari.
- (b) Serikali hupata ushuru.
- (c) Njia ya kujitajiyarisha kwa haraka.
- (d) Ni aina ya burudani inapotokea katika T.V na redio.
- (e) Kampuni hizi huweza kufadhili michezo na elimu.
- (f) Husaidia kupitisha wakati.
- (g) Husaidia katika kuinua jamii au kuzalisha mali kwa mfano mshindi atawapa wengine ajira.

KUPINGA

- (a) Huchangia utovu wa nidhamu kwa mfano wizi ili wapate pesa za kushiriki katika michezo.
- (b) Kifilisisha jamii kwa sababu ya utegemezi.
- (c) Washiriki kutopanua mawazo yao ya jinsi ya kupata riziki.
- (d) Ni njia ya kuvunja sheria.
- (e) Kupotosha jamii kwa mfano, washiriki kutumia pesa mfano za kulipa karo na matumizi mengine kucheza mchezo.
- (f) Kuruhusu watu wa umri mdogo kushiriki.

(g) Huchangia wanafunzi kuacha shule.

(h) Hufanya vijana kuwa wavivu.

TANBIHI

Mwanafunzi anaweza kujitokeza na hoja nyingine yoyote mradi ni sahihi.

Mwanafunzi anastahili kutoa hoja za kuunga na kupinga kisha atoe msimamo wake. Msimamo uegemee upande ambao una hoja nyingi. Endapo atakosa kutoa msimamo atakuwa amepungukiwa kimtindo.

Endapo atatoa hoja zinazotoshana na asitoe msimamo wake basi aathibiwe kimtindo.

SWALI LA TATU

BENDERA HUFUATA UPEPO.

3(A) Bendera inawakilisha watawaliwa (wafanyikazi, waumini, wanafunzi, wananchi.)

Upepo ni ishara ya nguvu kwa hivyo, inasimamia (Viongozi wa serikali, dini, mashirika, shule n.k)

(B) Mhusika anayeiga matendo yanayofanywa na mwingine kwa mfano;

(i) Mtoto ambaye ni mlevi / kahaba / mwizi na anakuwa anafuata matendo ya mzazi.

(ii) Mhusika ambaye anaingilia tabia fulani kwa sababu ya rika / marafiki wake. Tabia yaweza kuwa nzuri au mbaya mradi marafiki wake wana tabia ile.

(C) Amri inayotolewa na kiongozi wa (Taifa, shule, dini mashirika) na lazima kila mtu aifuate.

(D) Ikiwa mtahiniwa ataandika kisa ambacho mhusika anaenda kinyume na methali sharti aonyeshe adhabu inayompata mhusika, ikiwa hakuna adhabu basi mtahiniwa atakuwa amejitungia swali.

Kwa mfano, mhusika anayekataa kufuata amri k.v za shule, mwishowe afukuzwe shuleni.

SWALI LA NNE.

1.Suala litakalozungumziwa liwe ni jambo linalomgusa mhusika au kumwathiri.

2. Jambo lenyewe liwe linamgusa mzazi (baba) kwa kuwa anaona mwanawe anatabika na angetaka achukue hatua. Hatua hii ni kutatua tatizo/ shinda iliyopo. Mfano; amekawia kuoja/kuolewa na majukumu nyumbani yanamzidi.

3. Mhusika ashindwe kufanya uamuzi au atatizike katika kufanya uamuzi. Mhusika awe katika njia panda.

4. Mwanafunzi aweza kuendelea na kisa au akatumia mbinu rejeshi.

5. Katika kisa chake, atambulisha jambo linalozungumziwa. Mfano; ndoa, kurudi shule baada ya kuwacha masomo kwa muda.

TANBIHI

[DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM](http://EcoleBooks.com)

(i) Endapo mtahiniwa atakosa kwanza kwa maneno yale lakini kisa kinalenga atakuwa amepungukiwa kimtindo. Basi atuzwe alama zake.

(ii) Endapo mtahiniwa atakosa kuanza kwa maneno yale, na kisa kinalenga mada lakini ayapachike maneno yale popote atuzwe alama zake. Hata hivyo atakuwa amepungukiwa kimtindo.

(iii) Ikiwa ataanza kwa maneno yale lakini kisa kisilenge mada atakuwa amejitungia swali.